# AckySHINE.com

# Mahaba kwa wanawake wa siku hizi

By SW - Melkisedeck Shine · October 13, 2015

Baini Siri za Familia, Mapenzi na Mahusiano · #Karibu AckySHINE · #Mahusiano: Makala kwa Mke na Mume · #Mahusiano: Makala kwa Wanaume · #Mahusiano: Makala kwa Wanawake · #Mahusiano: Mapenzi ya Mbali · #Mahusiano: Uchumba na Urafiki · #SMS, Vichekesho, Mahusiano, Biashara na Ujasiriamali, Afya, Chemsha Bongo, Dini pamoja na Vitabu kwenye PDF

Wanawake wengi siku hizi hawajui au hawataki kuonesha mahaba Nimefanya kautafiti kangu kadogo nimegundua wanawake wengi siku hizi hawaonyeshi mahaba yani kwa ujumla hawako "Romantic". Wanawake wengi siku hizi akipata mwanaume anaona amepata mtu wa kumsaidia shida zake kwa hiyo hata akiwa ndani ya mahusiano anafikiria zaidi kutatuliwa shida zake kuliko mahusiano yenyewe.

? Wanawake wa siku hizi wengi, kwa mfano umemtoa out kidogo mkapate walau msosi sehemu nzuri, mkianza kula mpaka mnamaliza hakumbuki hata kukulisha kidogo kimahaba. Unakuta anakula msosi kimpango wake utafikiri anakula na kaka yake. Mnatoka kidogo mnatembea unakuta anatembea na wewe utafikiri anatembea na kaka yake; yani unaweza ukamuacha nyuma kidogo au akawa mbele yako anashindwa kujiongeza kupitisha mkono wake kwenye kikwapa chako na kukushika kimahaba. ? Wakati mwingine anakuona jasho linakutoka usoni anashindwa hata kukufuta kimahaba anakutazama tu utafikiri wewe ni kinyago cha mpapure. Wakati anakuaga anaondoka utafikiri anamuaga kaka yake hakupigi hata busu. Mwanamke unazungumza nae hakushiki hata ndevu zako kimahaba, mwanamke unakuwa nae hakufunyii massage wala hakukati mara moja moja kucha zako kimahaba. ? Wakati mwingine unakuta umekaa nae mwaka mzima kwenye mahusiano lakini hajawahi kukwambia neno "Nakupenda"mpaka wewe uanze kumwambia kwanza. ? Wanawake wengi wa siku hizi wanapenda kudekezwa, kubembelezwa na kupewa pesa ndio maana wengi utasikia wakisema "nataka mwanaume Romantic na mwenye pesa" lakini hawajiulizi je, wao ni Romantic? Au sisi wanaume hatuhitaji hayo mahaba ya wanawake? ? Asili ya mwanamke ni mfariji mkuu wa mwanaume lakini siku hizi wanawake wengi wamekuwa stress kwa wanaume. ? Note: Hakuna mwanaume mbahili kwa mwanamke Romantic.

Yafahamu Mambo Mbalimbali kuhusiana na Wanawake kwa Ku-Download Kitabu cha SIRI ZA MWANAMKE

Kitabu hiki kina topiki Zifuatazo; 1. Mambo anayohitaji mwanamke kutoka kwa Mwanaume 2. Mambo yanayowavutia wanawake kutoka kwa wanaume 3. Mambo wanayoyapenda wanawake wakati wa kufanya mapenzi 4. Dalili za mwanamke kicheche 5. Maswali ya kujiuliza kama mwanamke anakupenda kwa dhati au anakudanganya 6. Tabia za mwanamke anayekupenda lakini hawezi kusema 7. Ishara za mwanamke aliyevutiwa na wewe 8. Dalili za mwanamke anayeelekea kukukubali 9. Mambo ambayo mwanamke hawezi kukwambia 10. Njia za kudumisha na kuamsha mapenzi na mwanamke

[products columns="2" ids="30827"]